Jina _____ Nambari _____

Sahihi _____

Tarehe _____

102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA
SAA: 1 ¾

KIBWEZI SECONDARY SCHOOLS EXAMINATION
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 1
SAA: 1 ¾

MAAGIZO
(a) Andika Insha mbili: Insha ya kwanza ni ya lazima.
(b) Kisha chagua insha moja nyingine kutoka hizo tatu zlizobakia.
(c Kila Insha isipungue maneno 400.
(d) Kila Insha ina alama 20
(e) Karatasi hii ina kurasa mbili zilizopigwa chapa.
(f) Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa. Sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Kijitabu hiki kina kurasa 2 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

INSHA

1. Hebu fikiria kuwa umekuwa ukiishi nchini Libya. Baada ya ghasia za kisiasa zilizoikumba nchi hiyo umeporwa kila kitu. Iandikie jamii yako ujumbe wa rununu ukieleza hali yako na masaibu yaliyokupata

2. Fafanua jinsi ufisadi umedhoofisha uchumi wa nchi yetu .

3. Sikio la kufa halisikii dawa.

4. Nilipiga magoti nikasali na kumshukuru Maulana (Imalizie Insha yako kwa maneno haya).

102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA

KIBWEZI SECONDARY SCHOOLS EXAMINATION
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 1

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

SWALI LA 1

1. Shida ya njaa k.m.f kupata chakula
2. Malazi / makazi
3. Usafiri
4. Mavazi
5. Magonjwa
6. Hofu
7. Ukosefu wa pesa za matumizi
8. Upweke
9. Kazi imekatika / masomo

Mtindo
- Ujumbe uanze kwa salamu
- Kujuliana hali.
- Mwenye kuandika atambulishe mahali alipo.
- Mwili / maudhui
- Tamati – apendekeze usaidizi wowote.
- Kutoka kwa familia / taifa (kosa usafiri)
- Mwenye kuandika ajitambulishe kwa wenye kutumiwa ujumbe.

SWALI LA PILI
Jinsi ufisadi umedhoofisha uchumi wa nchi yetu.

1. <u>Sekta ya usafiri</u>
   - Barabara mbovu zinachelewesha bidhaa kufika sokoni
   - Abiria kutofika kazini wakati ufaao
   - Magari mabovu kuruhusiwa kuwa barabarani na baadaye kusababisha ajali

2. <u>Nafasi za kazi / ajira</u>
- Nafasi za kazi zinawaendea wasiohitimu vilivyo kwa sababu ya ufisadi.

3. <u>Wizara za Serikali</u>
   - Pesa hazitumiki kwa miradi iliyokusudiwa bali huishia kwenye mifuko ya watu binafsi.

4. <u>Mashirika yasio ya kiserikali</u>
   - Watu wameanza kuunda mashirika bandia ili wanufaike kifedha.

Kijitabu hiki kina kurasa 2 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

5. <u>Mashirika ya Kifedha</u>
   - Bidhaa / mali ya watu imesombwa kwa sababu ya kushindwa kulipa mikopo. N.k

<u>SWALI LA 3</u>

Sikio la kufa halisikii dawa
Mwanafunzi atunge kisa kinachoafikiana na ukweli wa methali hiyo.

<u>SWALI LA 4</u>

- Hii ni Insha ya kubuni.
- Mwanafunzi yuko huru lakini ni lazima amalizie kwa maneno aliyopewa.

<u>Mada</u>
- Mtahiniwe azue mada mwafaka.

Jina _____ Nambari _____

Sahihi _____

Tarehe _____

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
SAA: 2 ½

KIBWEZI SECONDARY SCHOOLS EXAMINATION
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 2
SAA: 1 ¾

MAAGIZO

(a) Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(c) Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

SWALI	UPEO	ALAMA	
1	15		
2	15		
3	40		
4	10		
JUMLA			

Kijitabu hiki kina kurasa 10 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

A . UFAHAMU *(ALAMA 15)*

BORAMIMI NA NJUGU ZA NGWENJE

Babulao alifahamika na kila mtu katika eneobunge la Mipasho, kwanza kutokana na mwendo wake wa kuguchia na pili kwa faka yake kubwa ya kufuatilia masuala ya kisiasa. Tangu zamani alipokuwa mwanafunzi, Babulao alikuwa na ndoto ya kuwa mwansiasa mwenye kutajika. Baada ya hatima ya masomo yake, ndoto yake haikutimia lakini hakukata tamaa kuwa siku moja ataikata kiu yake ya uanasiasa.

Babulao alikuwa na kiredio chake kidogo alichokitumia kufuatilia habari muhimu za nchi na matukio ya kutwa kucha. Kila wakati alizunguka huku na huku amekibeba kiredio chake hicho. Alikuwa na tabia ya kujishaua kwa kuwauliza wanakijiji maswali mbalimbali ya kisiasa, “Unajua waziri amesema nini leo?” atamwuliza mmoja wao ambaye atajibu.

“Sijui mimi” Babulao ataangua kicheko na kusema, “Ahh, bora mimi na kiredio changu! Nafahamu habari zote tangu mwanzo mpaka aheri!” Atakutana na mwingine na kumwuliza, “Wajua Bwana DC alikuwa wapi leo?”

“Sijui mimi,” atajibiwa

Kisha atasema, :Aha, bora mimi na kiredio changu. Najua alipokuwa Bwana DC leo!” Watu wa eneo hili wakambatiza “Boramimi’ na jina lake la zamani likafilia majinani.

Maisha ya Boramini yalibadilika alipolipwa ridhaa kubwa kutoka shirika la reli alikoumia mguu wake. *Alizisarifu* pesa zake vyema; akajenga bahari ya nyumba kijijini na nyingine akaamua kuziweka akiba kwa nia ya kujiingiza kwenye siasa “Ninataka kuingia bungeni, nisikilizwe kwenye redio mimi mwenyewe!” Aliwaambia marafiki zake. Muda ni muda, habari zenyewe zikatangaa kijiji kizima kama pepo za chamchela. “Babu wee, Boramimi anataka kuwa mbunge!” Watu wakawa wanaambizana. Wengine walianza kudhihaki kuwa hakuweza kumudu kampeni za uchaguzi ambazo zilikuwa na kukuru kakara nyingi.

Harakati za uchaguzi zilipokaribia, Boramimi alifanya maandalizi yake ya uchaguzi. Hata hivyo, watu walisema kuwa hakuwa na uwezo wowote kwa sababu hakuwa na pesa za kutosha. Mpinzani wake, Mzee Ngwenje, alikuwa ameahidi kufanya kampeni ya mwaka kuhakikisha kuwa ameuhifadhi ubunge wake. Hata hivyo, licha ya kuwa alikuwa mbunge wa jimbo hilo kwa takriban miaka kumi, Mzee Ngwenje hakuwa amefanya lolote. Kila mara baada ya uchaguzi aliyoyomea mjini hadi uchaguzi mwingine ulipokaribia tena. Hamna aliyemsikia kwa la heri wala kwa shari. “Hata mimi sikumsikia kwenye kiredio changu! Boramimi aliwaambia watu.

Lakini Ngwenje naye alikuwa *gwiji* wa wajanja. Kila uchaguzi ulipokaribia alinunua magunia ya mahindi na kuyasambaza haraka haraka kwenye eneobunge lake. Ilitokea sadfa kuwa mara nyingi kulikuwa na njaa kubwa wakati wa uchaguzi. Watu walipopata mahindi hayo walimpigia Ngwenje kura naye akajisemea,

“*Wajinga ndio waliwao*!”

Lakini mara hii Mzee Ngwenje hakuwa na bahati kwa vile hakukuwa na njaa hata kidogo. Mvua za masika zilinyesha vyema na watu wakavuna mazao ya kazole. Mara hii ataniona, ni mimi na yeye!" alisema Boramimi. Ingawa watu hawakumpenda sana Boramimi, walimstahabu yeye kuliko Bwana Ngwenje. Jinsi kampeni zilivyoendelea ndivyo livyozidi kuonekana wazi kuwa huenda Boramimi akaibuka mshindi na Mzee Ngwenje kupoteza kiti chake cha ubunge. Ngwenje alipotambua kuwa watu walikuwa wakimshabikia Boramimi, alipigwa na butwaa. Sasa atafanya nini na watu hawakuwa na njaa? Atatumia ujanja gani tena? Ilibidi atafute mbinu mpya.

Siku mbili kabla ya uchaguzi, Ngwenje alifika kutoka jiji kuu na magunia mawili yenye vifuko vilivyokuwa vimefungwa kama mchele au sukari. Aliwachukua vijana kadha na kuwakabidhi mifuko hiyo ili kuwagawia vijana wenzao walioshirikiana nao kumpigia kampeni. Ndani ya vijifuko hivyo kulikuwa na njugu. Vijana wakashika safari na kutembelea kila kijiji kusambaza zile njugu. Watu walipogundua mipango yao wakawaambia, "Sisi si watoto wa kudanganywa kwa njugu; wapelekeeni watoto wa shule."

"Hizi si njugu za huku mashenzini; Hizi huipa miili nguvu mpya ya kuweza kushiriki katika harakati za kampeni; ni uvumbuzi mpya wa kisayansi. Ngwenje anataka tumfanyie kampeni kwa nguvu na msisimko ili akamilishe miradi aliyoianzisha," walisema. Vijana hawa wenyewe walikuwa wakizitumia

njugu hizo na kusisimkwa ajabu. Waliweza kuuponda wa fisi wakiimba nyimbo za kumsifu Ngwenje na kuwahimiza watu wampigie kura. Uvumi ulienezwa kuwa njugu hizo zilikuwa na uwezo wa kuituliza akili na kulainisha viungo vya mwili ajabu. Baadhi ya watu waliingiwa na hamu ya kujaribu njugu hizo za ajabu. Baadhi ya watu waliingiwa na hamu ya kujaribu njugu hizo za ajabu. "Ahh, si mbaya kama zinawatia watu hamasa ya kutenda kazi," wakasema kwa furaha. Hawa waliwashawishi wenzao wengine na kuunda kundi sawa na la vijana waliompigia ngwenje debe kwa msisimko mkubwa.

Boramimi alifanya juu chini akajipatia kijifuko kimoja na kukihifadhi. Kama kawaida yake hakusombwa wimbi la kuzijaribu njugu hizo. Siku ya uchaguzi ilipofika, Ngwenje akashinda kwa mara nyingine. Wakati huo Boramimi alikuwa kaondoka kuelekea jiji kuu, wengine wakituhumu kuwa alikwenda kufuatilia matokeo ya uchaguzi akishuku kuwa huenda walimrubuni. Haukupita muda Boramimi akafika nyumbani akiandamana na watu kadhaa aliowakabidhi kile kijifuko cha njugu. Ngwenje akakamatwa mara moja na kutiwa ndani akingojea mashtaka. Watu walipigwa na butwaa kubwa kisha kimya kirefu kabla ya kusema, "Ahh Babu wee … Bora alaa!"

Tangu siku hiyo Bobulao akawa shujaa wa eneobunge zima. Na katika uchaguzi wa marudio uliofanywa baada ya kisa hicho, Babulao akapata ushindi mkubwa na kuwa mbunge mpya wa eneobunge la Mipasho.

Maswali

(a) Eleza ni kwa nini Babulao akaitwa Boramimi? (alama 2)

_____
_____
_____
_____

(b) Ni kwa nini watu walidhani kuwa Bw. Boramimi hangeweza kushinda uchaguzi. (alama 2)

_____
_____
_____
_____

(c) Ni kwa nini Mzee Ngwenje hakuwa na bahati katika uchaguzi uliokuwa unawadia? (alama 2)

_____
_____
_____
_____

(d) Uvumi wa njugu za Mzee Ngwenje ulienea kila mahali kuwa zilikuwa na uwezo gani? (alama 2)

_____
_____
_____
_____

(e) Wajinga ndio waliwao. Methali hii ina uhusiano gani na kifungu hiki? (alama 2)

_____
_____
_____
_____

(f) Ni kwa nini Mzee Ngwenje alikipoteza kiti chake cha eneo bunge la Mipasho? (alama 2)

_____
_____
_____

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu

(i) Gwiji (alama 1)

_____
_____
_____

(ii) Sarifu (alama 1)

_____
_____
_____

(iii) Bahari ya nyumba (alama 1)

B. MUKTASARI

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuataia.

Mwaka wa 1978 utakumbukwa kwa karne nyingi nchini Kenya. Huu ndio mwaka ambao Mtukufu Rais Daniel Toroitich Arap Moi alitangaza vita dhidi ya kutojua kusoma na kuandika. Mwaka huo pia alitangaza kuanzishwa kwa mpango wa maziwa ya bure kwa watoto wa shule za msingi na kutilia mkazo elimu ya watu wazima kote nchini.

Tangu wakati huo, katika kila kata ndogo, mtaa,kijiji, wilaya, miradi ya masomo ya watu wazima imestawi na kutekelezwa barabara,. Serikali imesisitiza umuhimu wa kila mtu mzima kujua kusoma na kuandika. Mafanikio yake kwa mtu binafsi na taifa zima hayana kipimo. Jambo la kwanza muhimu ni kuhifadhi siri kwa mtu binafsi. La pili kustawisha mawasiliano kwa taifa nzima kuendeleza utamaduni wetu na kukuza uchumi wa nchi yetu.

Maendeleo mengi kutokana na miradi ya elimu ya watu wazima yamepatikana kote nchini. Magazeti ya mikoani kama vile *Nyota ya Mashariki, Sauti ya Kericho* na mengine yanayochapishwa pwani na Mkoa wa Nyanza ni ya kutia moyo. Mbali na kuchochea ari ya kusoma, magazeti haya yameajiri wananchi wengi kazi, huku yakipiga vita kutojua kusoma na kuandika.

Kutokana na harakati hizi, makundi mengi ya akina mama yameundwa. Makundi haya yana lengo kubwa la kuinua uchumi wa nchi pamoja na kuinua afya ya taifa zima. Akina mama wanapokutana aidha wana mazungumzo kuhusu chakula bora kwa jamii au wana shughuli za kuunda bidhaa za kuuza. Tangu kuanzishwa kwa mpango huu, jamii nyingi zina afya bora kwa watoto na hata watu wazima. Akina mama wamefunzwa maana ya chakula bora.

Isitoshe, miradi ya ukulima na ufugaji kwa makundi haya ya akina mama imetia fora. Makundi mbalimbali yana mipango tofauti tofauti. Kuna wale wanaofuga kuku wa nyama na wa mayai. Kuna wengine wanaofuga nguruwe, mbuzi au hata kukuza mboga kulingana na mazingira. Wengine wana miradi ya kujenga nyumba za kukodi au kufuma mikeka, vikapu, vinyago na nguo. Shughuli hizi zote bila shaka zimeleta mafanikio makubwa.

Hata hivyo, mafanikio hayaji bila matatizo. Tatizo moja kubwa ni la kimawazo. Kunao wenzetu ambao wangali na fikira za kizamani. “Ikiwa hatukujua kusoma na kuandika wakati wa utotoni, hatutaweza tukiwa na umri wa makamo.” Wazo hili si sahihi. Wako ambao huanza kusoma wakiwa watu wazima na kuendelea hadi chuo kikuu.

Tatizo linalokumba mpango wa elimu ya watu wazima ni kutoshiriki kwa akina baba wengi kwa sababu wanadhani kwamba mke akimshinda mume itakuwa aibu. Mara nyingi kuna ukosefu wa vifaa. Kwa bahati nzuri

shule nyingi za msingi zimetumiwa kama vituo vya masomo ya watu wazima. Ingawa hivyo, uhaba wa vitabu na walimu waliohitimu ni mambo yatakayotatiza mpango huu kwa muda. Serikali yetu iko mbioni kushughulikia mipango hii, ambayo imetambuliwa kuwa muhimu sana kwa maendeleo ya taifa la Kenya.

Maswali.

(a) Eleza mafanikio ya elimu ya watu wazima. (maneno 55-65) (alama 10)
Matayarisho

Nakala safi

5.

(b) Ni matatizo gani yamekumba mipango ya elimu ya watu wazima? (maneno 25-30) (alama 5)
Matayarisho

Nakala safi

_____
_____
_____
_____

6.

3. Matumizi ya lugha

(a) Taja sauti zozote mbili za ufizi. (alama 2)

_____
_____
_____
_____

(b) Bainisha aina za maneno katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Ng'ombe huyu alinunuliwa jana.

_____
_____
_____
_____

(c) Changanua viambishi katika neno lifuatalo. (alama 3)
Nitamchezea

_____
_____
_____
_____

(d) Andika kwa wingi
Yeye hataki kucheza na mtoto aliye na kidole kichafu. (alama 2)

_____
_____
_____
_____

(e) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya mshazari. (alama 2)

_____
_____
_____
_____

(f) Andika sentensi ifuatayo kwa hali ya udogo na wingi. (alama 2)
Mtu huyu amejenga nyumba yenye milango ya mti.

_____
_____
_____
_____

7.

(g) Unda nomino kutokana na nomino zifuatazo. (alama 2)
(i) Mbabe
(ii) Shujaa

_____

_____
_____
_____

(h) Changanua sentensi ifuatayo kwa mishale.
Mwanariadha bora alijizolea hela nyingi sana ingawa alishindwa kuyamudu maisha yake. (alama 4)

_____

_____	_____
_____	_____
_____	_____
_____	_____
_____	_____
_____	_____
_____	_____

(i) Tambua shamirisho kipozi na shamirisho kitondo. (alama 2)
(i) Mtoto alimshika paka mkia.

_____
_____
_____
_____

(j) Taja visawe vya maneno yafuatayo. (alama 2)

(i) Mjinga _____

(ii) Ndovu _____

(k) Eleza matumizi ya <u>ku</u> katika sentensi zifuatazo. (alama 2)
(i) Ninakutaka ufike hapa

_____
_____
_____

(ii) Kwenye miti hakuna wajenzi

_____
_____
_____

(l) Tunga sentensi kuonyesha matumizi sahihi ya viunganishi vifuatavyo.
(i) Wala (alama 2)

_____
_____
_____

(ii) Sembuse / seuze (alama 2)

_____
_____
_____

(m) Tambulisha aina za nomino zilizopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo. (alama 2)
(i) <u>Amani</u> haiji ila watakapoelewana

_____
_____
_____
_____

(ii) <u>Kuondoka</u> kwake kulileta hasara kubwa.

_____
_____
_____

_____

(n) Tunga sentensi kwa kutumia neno huyu kama :- (alama 2)

(i) Kiwakilishi

(ii) Kivumishi

_____

_____

_____

_____

(o) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika hali zilizopendekezwa. (alama 3)

KITENZI	KAULI	JIBU
(i) Funga	Tendata	_____
(ii) Nywa	Tendeshea	_____
(iii) Paka	Tendea _____	

(p) Yakinisha sentensi ifuatayo. (alama 2)

Mvua haijanyesha vizuri msimu huu.

_____

_____

_____

_____

(q) Andika kinyume cha maneno haya. (alama 2)

(i) Kwama _____

(ii) Angika _____

4. ISIMU JAMII

(a) Eleza sababu zozote sita zinazochangia kufa kwa lugha. (alama 6)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

(b) Taja mambo yoyote manne yanayofanywa na serikali yetu kuimarisha lugha ya Kiswahili. (alama 4)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
SAA: 2 ½

KIBWEZI SECONDARY SCHOOLS EXAMINATION
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

Ufahamu
(a) Kutokana na tabia yake ya kusema Boramimi na kijiredio changu baada ya kuwauliza maswali na kushindwa kujibu. (alama 2)

(b) (i) Hakuwa na uwezo wowote wa kifedha.
(ii) Mpinzani wake alikuwa ameahidi kufanya kampeni ya mwaka. (alama 2)

(c) (i) Hakukuwa na njaa
(ii) Kulikuwa na mvua ya masika na watu wakavuna mazao mengi.

(d) (i) Uwezo wa kuituliza akili
(ii) Kulainisha viungo vya mwili ajabu. (alama 2)

(e) Mzee Ngwenje alikuwa anawatumia wakaazi wa eneo bunge lake kuwahonga kwa mahindi. Baada ya kunyakua kiti, alitorokea mjini na kuwasahau. (alama 2)

(f) (i) Njugu alizokuwa akiwapa watu zilithibitishwa kuwa zilikuwa dawa za kulevya.
(ii) Ngwenje alikamatwa mara moja na kutiwa ndani.

(g) (i) Mtaalamu / shujaa / mwenye ujuzi
(ii) Hifadhi / tunza vizuri
(iii) Nyumba kubwa

2. MUHTASARI
Majibu

(a) -Makundi mengi ya akina mama yameundwa
- Makundi haya yameinua uchumi wa nchi
- Miradi ya kilimo na ufugaji kuanzishwa
-Jamii nyingi zimeimarisha afya bora kwa watoto na watu wazima
- Magazeti mengi yamechapishwa
- Magazeti yameajiri wananchi wengi zozote 5 x 2 = 10

(b) -Tatizo la kimawazo
- Akina baba kuogopa kushindwa na akina mama
- Ukosefu wa vifaa
- Uhaba wa walimu waliohitimu Zozote 3 x 1 = 3

- Utiririko
- Kila kosa la sarufi / tahajia liadhibiwe (alama 2)

3. MATUMIZI YA LUGHA

(a) /d/, / t/ , / n/ , / l / nk (alama 2)
(b) N + V + T + E (alama 2)
(c) Ni – nafsi
ta – wakati
m – kitendewa
chez – mzizi
e – kauli
a – kiishio (alama 3)

(d) Wao hawataki kucheza na watoto walio na vidole vichafu. (alama 2)

(e) (i) Kuonyesha kumbukumbu au tarehe
k.m kumb / 1 / 2011
(ii) Kuonyesha maneno Fulani yako na maana sawa mf. Watu / binadamu
(iii) Kuonyesha hali mf. Mbuzi / sungura (alama 2)

(f) Vijitu hivi vimejenga vijumba / vyumba vyenye vijilango vya vijiti. (alama 2)

(g) Ubabe / mibabe
Ushujaa / mashujaa (alama 2)

(h) S → S^1 + U + S^2
S^1 → KN + KT
KN → N + V
N → Mwanariadha
V → Bora
KT^1 → T + N + V + E
T → Alijizolea
N → Hela
V → Nyingi
E → Sana
U → Ingawa
S^2 → T + T + N + V
T → Alishindwa
T → Kuyamudu
N → Maisha
V → Yake

(alama 4)
Kila kipengele ¼

(i) Kipozi – Mkono
Kitondo – Mkia (alama 2)

(j) Juka / Bora
Tembo (alama 2)

(k) (i) Nafsi ya pili umoja (wewe)
(ii) Mahali (alama 2)

(l) Kuhakiki jibu la mwanafunzi (alama 2)

(m) Dhahania
Kitenzi jina (alama 2)

(n) Hakiki majibu ya mwanafunzi (alama 4)

(o) (i) Fungata
(ii) Nyweshea
(iii) Pakia (alama 3)

(p) Mvua imenyesha vizuri msimu huu. (alama 2)

(q) (i) Kwamua
(ii) Angua (alama 2)

4**. MAJIBU YA ISIMU JAMII**

(a) Kiuchumi
Maendeleo na ubunifu wa viwanda yanafanya watu kuhamia mijini. Watu wanapohamia mijini wanaacha kuzungumza lugha moja na kuanza kuzungumza nyingine kwa ajili ya mawasiliano.

(b) Uchache wa wazungumzaji
Idadi ya watu wanaozungumza lugha Fulani inapopungua, lugha hiyo inakabiliwa na tisho la kufifia.

(c) Kutoungwa mkono na taasisi mbalimbali
Lugha yoyote isipoungwa mkono na taasisi kama elimu, dini na vyombo vya habari hukabiliwa na tisho la kufa.

(d) Hadhi
Lugha ambazo hazina hadhi kuishia kufa.

(e) Ndoa za mseto
Watu wanapochanganyikana kupitia ndoa za mseto husababisha lugha zingine kudidimia. Hii ni kwa sababu watoto huzungumza lugha ya mama kwa maana ndiye anakaa nao kwa muda nrefu.

(f) Kuhama kwa watu
Watu wanapohama kutoka sehemu moja hadi nyingine, lugha zao huathiriwa kwa kasi. Wengine husahau lugha zao kabisa.

(g) Sababu za kisiasa
(h) Athari za elimu

Zozote 6 x 1 = 6

(b) Mambo manne
1. Kiswahili kufanywa lugha ya Taifa / Rasmi
2. Katiba ilipitisha Kiswahili kiwe lugha rasmi nchini.
3. Kiswahili kufanywa somo la lazima shule za upili / msingi
4. Shughuli za bunge kuendelezwa kwa lugha ya Kiswahili.
5. Vyombo vya mawasiliano kutumia lugha ya Kiswahili
6. Vitabu vingi kuchapishwa kwa lugha ya Kiswahili (Hoja zozote 4 x 1 = 4)

Jina _____ Nambari _____

Sahihi _____

Tarehe _____

KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
SAA: 2 ½

KIBWEZI SECONDARY SCHOOLS EXAMINATION
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 3
SAA: 2 ½

MAAGIZO

(a) Jibu maswali manne pekee.
(b) Swali la kwanza ni la lazima .
(c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Ushairi, Tamthilia, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.
(d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
(e) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Kijitabu hiki kina kurasa 3 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

SEHEMU A: KW WAMITILA
MAYAI WAZIRI WA MARADHI na Hadithi Nyingine.

1. LAZIMA
(a) Matatizo ya kinyumbani ndiyo yalimfanya Likono apate ajali. Thibitisha kauli hii (alama 10)
(b) Eleza hulka za Bwana Kizito kibambo kama zinavyojitokeza katika kisa hiki. (alama 10)

UTENGANO – SAID A MOHAMED

2. "……, binadamu anaweza kuwa mnyama, lakini anaweza kurejea ubinadamu wake, na unapokuwa huna budi, ukatenda mambo wasiyoyapenda watu, watu huwa hawatazami sababu za wewe kutenda hivyo, bali tu watakupagaza unyama."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Fafanua kwa kutolea mifano kutoka kwa riwaya mambo sita anayeambiwa maneno aliyatenda. (alama 12)

(c) Mwafulani huyo alirejea ubinadamu wake vipi? (alama 4)

AU

3. (a) Taja sheria alizopewa Maimuna na mama Jeni za kuishi pale kwake wakati walipokuwa Cafe Afrique. (alama 6)
(b) Ni kitu gani kilichomfanya Maimuna kuhama kutoka kwa mama Jeni? (alama 4)
(c) Yataje matatizo yoyote matano Maimuna aliyokumbana nayo pale alipohamia. (alama 10)

TAMTHILIA : KITHAKA WA MBERIA
KIFO KISIMANI

4. "Bahati nasibu inapomteremkia mtu, mara nyingine uhalisi uonekana kama ndoto. Mambo huwa hayaeleweki kwa urahisi.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Ni nasibu gani iliyomteremkia anayeambiwa? (alama 2)
(c) Jadili hulka anayerejelewa. (alama 14)

AU

5. Jadili mchango wa vijana katika jamii ya Kifo Kisimani. (alama 20)

SHAIRI
6. ***Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata.***

1. Waume msiudhike, swali nawauliza,
Wala msibabaike, hadhi yetu watetea,
Kuwatweza wanawake, hamuoni mwakosea?
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

2. Si vizuri kuwatesa, wanawake kuonea,
Kuwapinga pasi kosa, kwa hakika ni hatia,
Nyote mna sawa hisa, katika hii dunia,
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

3. Mngakaa mfikiri, lau kwa miaka mia,
Na muwache ujabali, wanawake si ngamia,
Sidanganywe na mahari, msambe ni kununua,
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

4. Madhara huwa mengi, kwa waume narudia,
Hawawekea vigingi, wanawake kila njia,
Kwa waume hawasongi, fikira zao kutoa,
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

5. Usawa tunaotaka, si wa umbo na kuvaa,
Wala si wa kugeuka, kuota ndefu vifua,
Ni ule wa kutukuka, kwenye utu na tabia,
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

6. Waume vuta akili, nguvu si kujivuma,
Mwapaswa kubadili, dhana zenu na tabia,
Hakuna mtu dhalili, elimu yetu sawia,
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

7. Nimeutaja usawa, nadhani mmesikia,
Kama sahani na kawa, pima utu na hisia,

Kwa ujenzi twatakiwa, kina mama na raia,
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

Maswali

(a) Ipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 1)

(b) (i) Shairi hili ni la aina gani? (alama 1)

(ii) Jadili muundo wa hili sahiri. (alama 4)

(c) Dhihirisha jinsi mshairi (mtunzi) alivyoutumia uhuru wake wa utunzi. (alama 2)

(d) Kwa mujibu wa hili shairi kwa nini mtunzi analalamika? (alama 5)

(e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(f) Eleza maana ya misemo ifuatayo kama ilivyotumiwa katika shairi hili. (alama 3)
(i) Kuwatweza
(ii) Vigingi
(iii) Kuwapinga pasi kosa. (jumla 20)

FASIHI SIMULIZI

7. (a) Eleza maana ya misimu. (alama 2)
(b) Jadili hoja zozote tano zinazochangia katika uundaji wa misimu. (alama 10)
(c) Eleza sifa za misimu. (alama 8)

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI

KIBWEZI SECONDARY SCHOOLS EXAMINATION
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 3

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

Swali la 1

(a) (i) Mshahara wa Likono ulikuwa mdogo.
(ii) Likono ni mtu mwenye madeni mengi mno.
(iii) Watoto wa Likono wamekosa sare za kwenda shule.
(iv) Mavazi ya Likono ni duni – kmf Ni magwanda yaliyopauka rangi.
(v) Familia ya Likono inategemea mshahara duni kwa chakula, kodi ya nyumba n.k.
(vi) Likono anashindwa kujilipia gharama ya hospitali.
(vii) Watoto wa Likono walifukuzwa shuleni alipokuwa hospitali.
(viii) Mkewe alikuwa amestaafu.
(ix) Mtoto wake Rita hajapata kazi.
Zozote Hoja 5 x 2 = 10)

(b) (i) Ni mwenye maringo.

(ii) Hana utu kmf hakujali Likono.
(iii) Ana dharau dini km Anarejelea kisa cha Biblia kama tendo la zamani za kale.
(iv) Ni tajiri kmf ana gari.
(v) Ni mwongo kmf alidaganya kuwa alimkuta Likono barabarani ameanguka .
(vi) Ni mjanja

(Zozote 5 x 2 = 10)

UTENGANO – Said A. Mohamed

2. (a) - Maneno haya yalisemwa na Kabi.
- Alikuwa akimwambia Maimuna.
- Walikuwa katika ufuo wa bahari.
- Wakati Maimuna alikutana na Kabi mara ya pili.
- Maimuna alikuwa amemwambia yeye ni ndebe mbovu.

(Hoja zozote 4 x 1 = 4)

(b) (i) Kutoroka kwao nyumbani.
(ii) Kushiriki katika ukahaba.
(iii) Kushiriki katika ulevi.
(iv) Kupigana na watu kmf kidawa
(v) Kumtusi babake na kumfukuzilia mbali akiwa na Musa.
(vi) Kucheza densi huko Rumbalola .
(vii) Kutafeli watu kmf Mwenye duka.

Zozote 6 x 2 = 12

Kijitabu hiki kina kurasa 4 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

(c) - Aliolewa na Kabi.
- Akatulia kama mke.

(Zozote 2 x 2 = 4)

3. (a) (i) Chumba alichoonyeshwa ndicho kitakuwa chake.
(ii) Ikiwa ana shida amweleze mama Jeni.
(iii) Maimuna ajue kuwa wanasakwa na polisi.
(iv) Kazi ya ukahaba ni kazi .
(v) Atakachopata Maimuna kutakuwa na fungu la mama Jeni.
(vi) Maimuna asimlegezee mtu kmf pesa aziweke mbele.

6 x 1 = 6

(b) (i) Wivu
(ii) Wuzigiziwa wizi 2 x 2 = 4

(c) Taja matatizo aliyokumbana nayo pale alipohamia
(i) Elevi kmf palijaa walevi.
(ii) Uchafu kmf chumba alichopewa Maimuna kilijaa panya.
(iii) Kulikuwa na watu wachafu wenye tabia mbaya.
(iv) Milango ya chumba alichopewa ilikuwa imezeeka.
(v) Gondoro lilikuwa limezeeka.
(vi) Kulikuwa na kunguni.

Zozote 5 x 2 = 10

TAMTHILIA: KIFO KISIMANI
KITHAKA WA MBERIA

Majibu
4. (a) - Msemaji ni Mweke.
- Alikuwa akimwambia Gege.
- Ni mzungumzi nafsia wa Mweke / mawazo .
- Mweke ako kwa ukumbi.
- Anapanga jinsi ya kumshawishi Gege akubali kuondoa mwiba kwenye mguu wa Butangi.

(Hoja zozote 4 x 1 = 4)

(b) - Kuozwa Alida bintiye Mtemi Bokoni. (alama 2)

(c) Hulka ya anayerejelewa
(i) Tamaa
(ii) Mpenda anasa / mpenda raha
(iii) Mbinafsi
(iv) Msaliti
(v) Mjinga
(vi) Mwanamziki
(vii) Mvuvi
(viii) Katili
(ix) Muuaji Zozote 7 x 2 = 14

5. **MCHANGO WA VIJANA KATIKA TAMTHILIA YA KIFO KISIMANI**
(i) Kuwaza kuhusu maisha ya uma.
(ii) Kupigania ukweli.
(iii) Kupigania kuhusu amani.
(iv) Wanapinga mateso.

(v) Kuwaunganisha vijana wenzao kupinga maovu yanayoendelezwa na viongozi.
(vi) Wanatetea uhuru.
(vii) Wanatetea haki na heshima ya kila Mwanabutangi.
(viii) Wanataka kutatua matatizo ya raia.
(ix) Wanawazindua wananchi kuhusu haja ya utawala mzuri / unaofaa.
(x) Wanahimiza maendeleo ya nchi.
(xi) Wanahimiza usawa.
(xii) Wanalinda nchi.
(xiii) Wanaleta mapinduzi.

Zozote 10 x 2 = 10

SHAIRI

6. (a) - Usawa
- Wanawake wawe sawa na wanaume
- Tuache kuwadhulumu wanawake. Yoyote 1 x 1 = 1

(b) (i) Tarbia / unne / (kiarudhi) (alama 1)
(ii) - Beti saba
- Kila ubeti una mishororo 4.
- Kila mshororo una vipande viwili / ukwapi na utao
- Mizani katika kila mshororo
8 8 = 16
- Vina mg ubeti 1
Ke za
Ke ea
Ke ea
Wa ni
- Kibwagizo – wanawake wawe sawa, na waume duniani.

Zozote 4 x 1 = 4

(c) Uhuru wa mshairi
- Inkisari mf - Mngakaa
- Sidanganywe
- Msambe
- Kawa
- Kutaja √1
Mfano √ √2

(d) (i) Wanawake wanatwezwa / teswa

(ii) Wake wanachukuliwa kama vyombo vya kununuliwa kwa mahari.
(iii) Wawekewa vikwazo vingi
(iv) Wote wanaumbwa na Mungu / wote ni wanadamu.
(v) Maonevu / wanawake kuonewa / wanawake kupingwa pasi kosa.

5 x 1 = 5

(e) - Mkifaa na kufikiria hata kama ni baada ya miaka mia.
- Na muache kutumia nguvu kwani wanawake si sawa na ngamia.
- Msifikirie kwamba mnapowalipia mahari mnawanunua.
- Wanawake sharti wapewe usawa na wanaume duniani. (√ alama 4)

(f) (i) Kuwatweza – Kuwadharau / vunjia heshima.
(ii) Vigingi – vizuizi / vikwazo.
(iii) Kuwapiga pasi kosa – kutokubali mawazo ya wanawake hata ikiwa wayasemayo ni kweli

(√ 3 x 1 = 3)

7. FASIHI SIMULIZI

(a) Maana ya Misimu
- Maneno yanayozuka na kutumiwa katika mazungumzo na makundi maalum ya watu katika jamii.

(alama 2)

(b) Uundaji wa misimu
(i) Kufupisha maneno.
(ii) Kutohoa maneno ya kigeni.
(iii) Kutumia sitiari au jazanda.
(iv) Kutumia tanakali.
(v) Maneno kupewa maana mapya.
(vi) Kuunda maneno mapya

(Hoja zozote 5 x 2 = 10)

(c) Sifa za misimu
(i) Kuzuka na kutoweka baada ya muda.
(ii) Baadhi ni maneno yasiyo sanifu.
(iii) Ni lugha ya mafumbo.
(iv) Maneno huwa na maana nyingi.
(v) Baadhi ya maneno huweza kuingizwa katika lugha sanifu.
(vi) Maneno hugawika katika makundi mbali mbali.

(Hoja zozote 4 x 2 = 8)

4.